

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Anwani ya Simu: "REGCOM"
Simu: 028-2500690-2500686
Fax : 028-2501057/2541242
E-mail: ras.mwanza@tamisemi.go.tz
www.mwanza.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOA
S.L.P. 119,
MWANZA.

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

Ndugu zangu waandishi wa habari, tumeitana hapa kwa dhamira moja kubwa, kama mnavyo fahamu Mh. Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais Jamhuri ya Muungano Tanzania wakati aliposhiriki kwenye mazoezi ya pamoja na wanachi wa mkoa wa Dar es- Salaam yaliyokuwa yameandaliwa na wizara ya afya siku ya tarehe 17 Desemba, 2016, alitoa maelekezo ambayo ilitakiwa kila mkoa kuwa na Programme maalum ya mazoezi kila juma la pili la mwezi ili kuweza kuwafanya wafanyakazi na hata watu wengine ambao si wafanyakazi kushiriki kwa shabaha yakuimarisha afya zao.

Kufuatia agizo hilo na pia ikizingatiwa ongezeko la magonjwa yasiyo ambukiza kufikia asilimia 47 kote nchini, sisi kama mkoa wa Mwanza tumeazimia kutenga siku hiyo mara baada yakupokea ngazi ya taifa, ambapo pamoja na mazoezi hayo vile vile siku hiyo tutakuwa na wataalam wa afya ambao watakuwa wakipima afya zetu hasa kuhusiana na magonjwa yasiyo ambukiza..

Kwa nafasi hii niombe kupitia kwenu, muweze kutufikishia taarifa hizi kwa umma kwamba, siku ya Jumamosi tarehe 11 Februari, 2017 watumishi kutoka Ofisi na taasisi zote za Umma na zisizo za umma kufika katika

viwanja vya Furahisha kuanzia saa 12.30 asubuhi kwa ajili ya uzinduzi, ambao utaongozwa na Mh. John Mongella Mkuu wa Mkoa wa Mwanza. Ambapo kwa mwezi huu wa pili tutaongozwa na kauli mbiu **"Afya yangu Mtaji wangu, nafanya mazoezi kuilinda afya yangu"** lakini ifahamike kuwa kila mwezi tutakuwa na kaulimbiu mahususi kwa mwezi husika.

Lingine ambalo ningependa mfahamu ni kuwa, maandalizi yote muhimu kwa ajili ya siku hiyo yapo tayari, ikiwepo mialiko kwenda kwenya taasisi zote za umma na zisizo za umma, wataalam wa afya kwa ajili ya upimaji afya, Vifaa vya mazoezi na walimu wa mazoezi tayari wametayarishwa kwa ajili yakufanikisha katika siku hiyo

Katika Uzinduzi huo tutakuwa na matembezi ya pamoja, yatakayo anzia Viwanja vya Furahisha, kwenda hadi kona ya Bwiru kisha kuelekea kona ya Kitangiri na badaye kurejea tena Viwanja vya Furahisha kwa ajili ya Mazoezi ya Viungo yatakayo ongozwa na Wataalam na walimu wa Mazoezi ya Viungo kutoka katika vituo vyetu vya mazoezi (Gym) za hapa Mwanza.

Rai yangu niwaombe tujitokeze kwa wingi siku hiyo ya jumamosi, kwani sote tunafahamu afya zetu ndio mitaji yetu katika utendaji kazi.

Asanteni sana kwakunisikiliza.

Imetolewa na

Atley J. Kuni

Kny. Katibu Tawala Mkoa

Mwanza